



Taarifa kwa umma

Serikali inakusanya maoni ya wananchi kuhusu utoaji huduma za afya, elimu na maji

Jumatano 12 Desemba, Dar es Salaam: Kama sehemu ya mchango wake katika Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP), Twaweza imezindua shindano litakalohusisha utoaji wa kompyuta ndogo (laptops) kwa washindi na kwa shule watakazozichagua. Washindi watakuwa wale watakaotoa maoni bora zaidi kuhusu namna huduma za afya, elimu na maji zinavyoweza kuboreshwa na mwananchi anapaswa kufanya nini kuleta mabadiliko.

Serikali ya Tanzania inakusanya maoni ya wananchi kuhusu namna ya kuongeza ubora, uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma hizo. Twaweza inasaidiana na Serikali katika jukumu hili, kwa kutumia njia ya utayarishaji machapisho-pendwa na kusaidia kupitia maoni hayo.

Wito kwa wananchi kutoa maoni utasambazwa kupitia vitabu milioni nne vinavyozungumzia masuala ya jamii pamoja na machapisho mengine ambayo yatasambazwa kote nchini. Katika kila robo ya mwaka 2013, mawazo bora zaidi yatatumika kuipa Serikali taarifa; zaidi ya hilo, watoa maoni bora watajishindia kompyuta za mkononi. Mawazo bora zaidi pia yatachapishwa mtandaoni na kupitia majarida, magazeti na vitabu.

Vitabu hivi vinavyobeba shindano vimetayarishwa kwa kushirikiana Tamasha, Asasi inayojishughulisha na masuala ya vijana. Vitabu hivyo vinatoa mtazamo wa vijana kuhusu masuala ya afya ya mama; mimba za utotoni; viwango vya ubora wa elimu; uwekezaji katika rasilimali; utawala na ushiriki wa vijana katika kutoa uamuzi na afya, usafi binafsi na usafi wa mazingira. Mada za vitabu hivyo zinalenga kusambaza matokeo ya tafiti na mtazamo wa vijana kuhusu masuala haya.

Mpango wa OGP ni jitihada ya kimataifa inayolenga kuzifanya Serikali ziwe wazi zaidi na zinazowaitikia wananchi, kwa kuhamasisha uwazi, kuwawezesha wananchi, kutokomeza rushwa, na kutumia teknolojia mpya ili kuimarisha utawala. Nchi 58 zimejiunga na OGP hadi sasa, Tanzania ikiwa mojawapo, na yenyewe pia ni mwanachama wa Kamati Ongozi ya OGP.

Unaweza kusoma zaidi kuhusu Mpango Kazi wa Tanzania katika OGP hapa: <http://tinyurl.com/OGPTZ-mpangokazi>. Mpango huu umetoa kipaumbele kwa utoaji huduma za msingi na upatikanaji wa taarifa kama nguzo kuu ya vuguvugu la Tanzania kuelekea kwenye Serikali iliyo wazi zaidi.

Rakesh Rajani, Kiongozi wa Twaweza, alisema: *“Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa wazi ni mkabala mpya wa utawala unaozingatia ubia kati ya wale wanaotawala na wale wanaotawaliwa ili kutafuta ufumbuzi kwa changamoto kubwa zaidi zinazotukabili. Kukusanya maoni ya raia kuhusu namna ya kuongeza ubora katika utoaji huduma ni hatua muhimu ya kwanza katika*



kuhakikisha kwamba dira hii inakuwa kweli na Twaweza inafurahi kuweza kusaidiana Serikali kwa kufanya wito huu kwa watu usambae zaidi ili kukusanya maoni.”

--- Ends ---

Kwa taarifa zaidi:

Risha Chande

Afisa Habari na Utetezi, Twaweza

baruapepe: rchande@twaweza.org | t: (+255) (0) 656 665 7559

Matini kwa Wahariri

1. Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Serikali kwa Uwazi (OGP) ulizinduliwa mwezi Septemba, 2011 ukiwa na wenyekiti wenza wawili, Rais Obama wa Marekani na Rais Rousseff wa Brazil, ambao kwa pamoja walitoa tamko la pamoja la ahadi ya nchi zinazoshiriki kufanya tawala zao ziwe wazi na zinazowajibika.
2. Katika mkutano mkuu wa mwaka wa kwanza, uliofanyika katika jiji la Brasilia, wawakilishi kutoka Tanzania wakiongozwa na Rais Jakaya Kikwete, waliungana na wenzao kutoka sehemu mbalimbali ulimwenguni, ili kuelezea dira na mipango ya kitaifa katika kufungua milango ya Serikali kwa raia. Kwa pamoja, Serikali za OGP zimeweza kutoa ahadi 300 tofauti.
3. Nchi (58) zinazoshiriki hivi sasa zina watu wapatao bilioni mbili, sawa na asilimia 25 ya idadi ya watu wote duniani.
4. Kwa taarifa zaidi kuhusu OGP, ikiwa ni pamoja na orodha ya nchi zinazoshiriki, tembelea www.opengovernmentpartnership.org
5. Ili kupata undani wa ahadi za Tanzania na tarehe ya mwisho ya kuwasilisha, tembelea www.opengovpartnership.org/countries/tanzania na <http://blog.opengovpartnership.org/2012/09/tanzania-ogp-update/>
6. Tamasha ni asasi iliyojikita katika kufanya kazi na vijana nchini Tanzania, kwa kuhakikisha kwamba mitazamo yao kuhusu maendeleo inasikika na kusaidia kujenga uwezo wao. www.tamashavijana.com
7. Unaweza kufuatilia kazi za Twaweza kupitia: Tovuti: www.twaweza.org; Ukurasa wa Facebook: Twaweza Tanzania; Anwani ya Twitter: @Twaweza_NiSisi
8. Vitabu vinavyozinduliwa na Twaweza vimeorodheshwa hapa chini na vitasambazwa kupitia shule na mitandao mingine.
 - Afya yafia wapi?
 - Bure bora?
 - Kodi ya mimba, nani alipe?
 - Rasilimali mali ya nani?
 - Shule ni elimu?
 - Ushirikishwaji ni ushiriki?

Unaweza kuvipata vyote kwa kuvipakua kutoka <http://twaweza.org/go/youth-booklets>